



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA RUNGWE




Tarehe: 21/10/2021

**TANGAZO LA ZABUNI YA KAZI ZA UFUNDI KWA AJILI YA UKARABATI WA
HOSPITALI YA WILAYA TUKUYU**

ZABUNI NA. LGA/071/2021/2022/RDC/W/17

1. Tangazo hili linafuatia Tangazo la Mpango wa Manunuzi wa Jumla (GPN) wa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe lililotolewa tarehe 28/07/2021 kupitia mfumo wa manunuzi kwa njia ya mtandao wa PPRA.
2. Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe inapenda kuzitangazia Taasisi za Serikali zenye sifa za Ujenzi wa Miundo mbinu ya Serikali kwa ajili ya Ukarabati wa Miundo Mbinu ya Hospitali ya Wilaya Tukuyu kwa njia ya Manunuzi ya "Force Account". Ukarabati wa Miundo Mbinu hii utahusisha ujenzi wa:-
 - a) Ukarabati wa Jengo la Wagonjwa wa Nje (OPD),
 - b) Ukarabati wa Wodi ya Wanawake
 - c) Ukarabati wa Wodi ya Wanaume
 - d) Ukarabati wa Wodi ya Grade A
 - e) Ukarabati wa Wodi ya Grade B
 - f) Ukarabati wa Jengo la Maabara
 - g) Ukarabati wa Jengo la Meno
 - h) Ukarabati wa Njia za Wapita kwa Miguu (Walkways)
3. Ushindani wa zabuni hii utakuwa wa kimipaka kwa taasisi pekee za Kiserikali (Restricted Tendering) kwa Taasisi zifuatazo:-
 - i. SUMA JKT, Ofisi ya Nyanda za Juu Kusini, S.L.P 618, Mbeya
 - ii. Wakala wa Majengo ya Serikali (TBA) wa S.L.P 6360, Mbeya
 - iii. Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST) S.L.P 131, Mbeya
 - iv. Shirika la Nyumba Tanzania (NHC) S.L.P Mbeya

4. Hivyo basi, Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Wilaya inawakaribisha Taasisi tajwa hapo juu kujaza nukuu msako za gharama za Ufundi tu na kisha kuwasilisha barua ya ofa na nukuu zilizojazwa na kufungwa kwa "seal" maalum zikiwa katika nakala mbili kupitia anwani ya: Katibu wa Bodi ya Zabuni, Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe, S.L.P 148, Tukuyu zikiwa zimeandikwa kuwa "Zisifunguliwe kabla au saa 5:00 asubuhi ya tarehe 26/10/2021. Na kwamba nukuu msako hizo zitafunguliwa muda huo huo mara baada ya saa 5:00 asubuhi kwa uwazi mbele ya Wawakilishi wa Taasisi tajwa hapo juu watakaopenda kuhudhuria hafla fupi ya ufunguzi huo.
5. Ofa zitakazoletwa mara baada ya muda wa mwisho wa uwasilishaji zabuni hizo na ambazo hazitatajwa wakati wa ufunguzi hazitapokelewa kwa ajili ya kuzifanyia uchambuzi kwa bila kujali sababu zozote zile.



Mchau, R.B

MKURUGENZI MTENDAJI (W)
HALMASHAURI YA WILAYA YA RUNGWE

MKURUGENZI MTENDAJI (W)
RUNGWE